# Handeni Yetu

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni. Julai- Septemba 2017 Toleo Namba 01

**JARIDA LA MWENGE WA UHURU 2017**

## Miradi ya maendeleo Mwenge wa Uhuru 2017 yang'ara Halmashauri ya Wilaya ya Handeni



Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Handeni Eng.Gabriel Robert ambaye ni mkuu wa Wilaya ya Korogwe akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuuwa Wilaya ya Kilindi kwenye mapokezi ya Mwenge wa Uhuru Kiwilaya

### YALIYOMO NDANI

Mradi wa Tanki la Kuhifadhia maji Kwedikabu.



Mradi wa Ghala la kuhifadhia mazao kwachaga.



**Mradi wa Hoteli ya KN SAFARIS iliyopo Mkata.**



Mradi wa Maabara ya Kisayansi Shule ya Sekondari Kwaluguru



Mradi wa jengo la upasuaji kituo cha afya Mkata



# TAHARIRI

# YALIYOMO

*Karibu mpenzi msomaji wa Jarida la Handeni yetu ,ambapo lengo la jarida hili ni kuonesha miradi mbalimbali iliyopitiwa na Mwenge wa uhuru kwa mwaka huu wa 2017 kwa kuangalia thamani yake na ushiriki kuanzia ngazi ya Serikali kuu hadi jamii.*

*Mwenge wa Uhuru ni nuru na ishara ya amani, utulivu, upendo na mshikamano katika jamii ya Watanzania na matunda yake huwanufaisha wananchi wote bila kujali Dini, Kabila, Rangi, Itikadi na Rasilimali.*

*Mwaka 2017 Mwenge wa Uhuru umepokelewa na kukimbizwa kwa kilomita 128 katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni na umepitia Miradi ya Maendeleo 8 yenye thamani ya Tshs 2,030,619,096/= katika sekta za Elimu, Afya, Kilimo, Maji na Ujasiriamali. Kati ya Miradi hiyo 5 imezinduliwa, 2 imewekewa mawe ya msingi, 1 umetembelewa na kukabidhiwa cheti cha utambulisho. Halmashauri Tsh.106,366,735/=, Serikali kuu Tsh.568,412,342,/= Nguvu za Wananchi Tsh. 383,745,607 /= na Wadau wa Maendeleo Tsh. 972,094,412/=.*




*DIRA(VISION)*

*Kuwa na jamii iliyoelimika na kuwa na maisha bora.*

*DHAMIRA (MISSION)*

*Kuipatia jamii ya Halmashauri ya Wilaya ya Handeni maisha bora kiuchumi kwa kutumia vizuri rasilimali zilizopo kwa kudumisha Utawala Bora ili kuboresha maisha ya jamii*

## LINATOLEWA NA:

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.
S.L.P 355
Handeni, Tanga
Email:ded@handenidc.go.tz
Tovuti: www.handenidc.go.tz
fcebook: handenidc
youtube: handenidc





# Mradi wa ufunguzi wa Bohari ndogo ya kuhifadhia dawa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni

Bohari hii ya dawa ilianzishwa mwezi Machi 2017. Lengo likiwa kurahisisha upatikanaji wa dawa muhimu kwa muda mfupi katika vituo vya kutolea huduma za afya na kuongeza idadi ya wanachama wa CHF

Kwa kutumia Bohari hii, dawa zinanunuliwa na kuhifadhiwa ambapo vituo vikiishiwa au kupungukiwa dawa kuchukua kwenye hii bohari ndogo na kulipa kwa fedha zilizopo katika akaunti za vituo husika kwenda akaunti ya CHF ya Halmashauri kulingana na gharama ya dawa zilizochukuliwa.

Gharama za uanzishwaji wa bohari hii ya dawa ni Tshs 338,254,890/=, ambapo Tshs 9,668,450 ni gharama ya ukarabati wa chumba na uwekaji miundombinu ya kuhifadhia dawa, na Tshs 328,586,440 ni gharama za ununuzi wa dawa na vifaa tiba. Fedha hizi zote ni michango ya wananchi kupitia Mfuko wa Afya wa Jamii, Bima ya Afya ya Taifa na fedha taslimu za malipo ya huduma(papo kwa papo) kwa wateja wasio wanachama wa mifuko ya Bima za Afya.
Halmashauri imeweka utaratibu mzuri wa uendeshaji wa Bohari hii, ambapo;-

Usimamizi na uendeshaji wa bohari hii ya dawa upo chini ya Mfamasia wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.
Vituo vya Afya na Zahanati vinaainisha mahitaji ya dawa na vifaa na gharama zake kisha kamati



Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni DK.Mgimba akisoma taarifa ya Mradi wa Bohari ndogo ya dawa iliyozinduliwa .

za kituo zinakaa na kuidhinisha malipo kwenda akaunti ya CHF ya Halmashauri ya Wilaya.
3) Halmashauri ya Wilaya inatumia fedha za akaunti ya CHF kuagiza dawa na vifaa MSD na kwa wazabuni wa Halmashauri kwa wakati.
Utaratibu huu umeongeza upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya huduma za Afya kutoka asilimia 68 hadi 81 kwa sasa




Jengo la bohari ndogo ya kuhifadhia dawa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

"Wagonjwa tunaowahudumia ndio waliotuajiri, tuache kufanya kazi kwa mazoea, wananchi wapate huduma bora na kwa usawan akwakutoa vipaumbele kwa makundi maalumu"Alisema Amour

# Mkimbiza Mwege Kitaifa Amepongeza Mradi wa Maabara ya Kisayansi Shule ya Sekondari Kwaluguru na Kutaka Kutunza miundombinu na Vifaa vilivyopo.



*Maabara ya Sayansi kwa masomo ya Baiolijia, fizikia na Kemia Shule ya Sekondari Kwaluguru.*

Mradi huu wa ujenzi wa Maabara tatu za sayansi (Fizikia, Kemia na Baiolojia) ulianza rasmi mwaka 2014. Lengo la mradi huu ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata elimu ya mafunzo ya masomo ya sayansi kwa vitendo ili kuongeza uelewa na ujuzi katika masomo ya Sayansi. Hadi kukamilika kwake umegharimu jumla ya Tshs 105,228,000/=

Katika kuhakikisha kwamba wananfunzi wanan=jifunza kwa vitendo hususani kwenye masomo haya ya sayansi mradi huu hadi kufikia ukamilifu michango mbalimbali imetumika kuanzia Serikali kuu ambapo ilichangia kiasi cha Tsh.31,228,000/=, Mchango wa Halmashauri ni kiasi cha Tsh.40,000,000/=, Mchango wa jamii ni Tsh.23,000,000/=, Mchango wa wazazi/walezi Tsh.2,000,000/= stofali (2,000) na Mgambo JKT (ufundi)Tshs 9,000,000/-

Mradi huu wa utanufaisha wanafunzi wa Shule hii ya Sekondari ya Kwaluguru yenye jumla ya wanafunzi 259 ambao wanafunzi wa kike ni 146 na wanafunzi wa kiume ni 113

Wanafunzi hawa wakipata elimu muhimu ya Sayansi watatumika katika kuliendeleza Taifa hasa kwa sekta za viwanda na kuendana na kauli mbiu ya Mwenge 2017 "Shiriki Kukuza Uchumi wa Viwanda kwa Maendeleo ya Nchi yetu"



Mtendaji Kata Kata ya Kwaluguru akisoma Taarifa ya Mradi

Aidha Mkimbniza Mwenge wa uhuru Kitaifa alitoa Rai kutunzwa kwa vifaa na miundombinu iliyopo kwenye maabara hiyo na kuwataka uongozi wa Halmashauri kuweka kipaumbele kwenye miradi ya maabara ambayo bado haijamalizika, imaliziwe ili kila shule ya Sekondari iwe na maabara iliyokamilika na hatimaye kuzalisha wanasayansi watakaosaidia kukuza uchumi wa Tanzania ya Viwanda.



Mwananfunzi wa Shule ya Sekondari Kwaluguru akifundisha kwa vitendo kwa Viongozi mara baada ya kufungua maabara hiyo na Mkimbiza Mwenge Kitaifa.

"Madaktari, manesi, wafamasia,enginia na wataalamu wote wa sayansi wanatokana na masomo ya sayansi, kwa kufungua maabara hii tunaimani itazalisha wanasayansi wengi ambao watakuwa na msaada mkubwa husについて kwenye kuelekea Tanzania ya uchumi wa viwanda" alisema Amour alipofungua maabara hiyo.

# Mradi wa Ghala la kuhifadhia mazao ulivyowapa fursa wakulima wa mazao mbalimbali Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

Halmashauri ya Wilaya Handeni ni miongoni mwa Halmashauri 77 nchini zinazotekeleza programu ya MIVARF (Marketing Infrastructure, Value Addition And Rural Finance Support Programme). Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa ghala la kuhifadhia mazao katika kijiji cha Kwachaga-Tuliani kilichopo Kata ya Kwachaga. Mradi huu ulianza mwezi Mei 2016 na kukamilika Agosti 2017

Hadi kufikia hatua hii, mradi umegharimu kiasi cha Tshs 456,949,000/- zilizotolewa na Serikali Kuu na wananchi wamechangia kutoa ardhi yenye ukubwa wa ekari 10 na nguvu kazi katika kusafisha eneo la ujenzi. Ghala hili lina uwezo wa kuhifadhi tani 2,000 (Gunia 20,000) za nafaka kwa wakati mmoja.

Kukamilika kwa mradi huu kunalenga kuwasaidia wakulima; Kuwa na usalama wa chakula kwa kuwapatia hifadhi bora ya mazao, Kuwasaidia wakulima kuuza mazao kwa kutumia vipimo sahihi, Kuboresha uzalishaji, kufikia masoko kwa urahisi, kuwa na nguvu ya kupanga bei yenye faida, Kuongeza thamani ya mazao ya wakulima kwa kupanga madaraja, kusindika na kufungasha na Kuwaunganisha wakulima na taasisi za fedha ili kupata fedha za kuendesha mfumo wa stakabadhi mazao ghalani.



Mwenge wa Uhuruukiwa tayari mbele ya ghala la kuhifadhia nafka tayari kwa kufunguliwa na mkimbiza mwenge kitaifa 2017.

Mkimbiza Mwenge wa Uhuru Ndg. Amour Hamad Amour amepongeza jitihada za ujenzi wa ghala la kuhifadhia mazao ambalo limedhihirisha namna ambayo wakulima wamethaminiwa kwa kupatiwa eneo la uhakika la kuhifadhia mazao yao.

Ametoa rai kuhakikisha miundo mbinu iliyopo kutunzwa na kuhakikisha wananchi na wakulima wanelemishwa juu ya umuhimu na faida za kuhifadhi mazao kwenye ghala ili, ghala hilo liweze kutumiwa kwa ufanisi hatimaye kutimiza malengo yaliyokusudiwa.



Muonekano wa Ndani wa Ghala la kuhifadhia Nafaka lililojengwa Kata ya Kwachaga Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

# Mradi wa Hoteli itayotoa malazi bora kwa wakazi wa Handeni na wageni ikiwa ni pamoja na fursa ya kazi kwa vijana.

,



Mwenge wa Uhuru ukiwa umefika eneo la KN SAFARIS Lodge tayari kwa kukabidhi cheti

KN SAFARI LODGE inamilikiwa na Apronius Mutalemwa Muzo yenye Cheti cha Usajili Namba 249223 cha tarehe 12/11/2012 kutoka kwa wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA - Business Registrations and Licensing Agency).

Ujenzi wa Hoteli hii ulianza mwaka 2014 katika kijiji cha Mkata Mashariki, Kata ya Mkata, Tarafa ya Mazingara Halmashauri ya Wilaya ya Handeni na ulikamilika mwezi Julai, 2017.

Miundombinu ya Hoteli hii ni pamoja na 1) Vyumba vya kulala wageni 24 (Ishirini na nne),

2) Mgahawa wa chakula wenye uwezo wa kuhudumia watu 50 (Hamsini) kwa wakati mmoja, na

3) Kisima cha kuvuna Maji ya Mvua na kuhifadhi lita Laki mbili (Lita 200,000).

***Mkimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa amepongeza miradi yote iliyofunguliwa, kuwekewa mawe ya msingi, kutembelewa na kukabidhiwa cheti.***




Wakimbiza Mwenge, viongozi, wataalamu mbalimbali na wananchi wakiingia ndani ya hoteli ya KN SAFARIS kutazama miundombinu iliyopo ndani ya hoteli hiyo.

Malengo ya KN SAFARI LODGE ni pamoja na Kutoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa vijana na wananchi kwa ujumla, kuwa kivutio na kuchochea utalii katika Wilaya ya Handeni, kutoa huduma za chakula na malazi bora. Katika sekta zingine, uwekezaji huu utasaidia kuongeza pato la Wananchi, Halmashauri na Taifa kwa ujumla.

Hoteli hii ya KN SAFARIS itaweza kuwasaidia wafanyabiashara mbalimbali wakaofika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni kufata bidhaa mbalimbali hususani za shambani kupata malazi ambayo ni bora na yaliyopo kwenye mwambao wa barabara kuu inayounganisha mikoa ya Kusini KilimanjaroArusha na Tanga.

# Ufunguzi wa Chumba cha upasuaji kituo cha afya cha Mkata chenye lengo la kuokoa maisha ya mama na mtoto.

Mradi huu wa ujenzi wa Jengo la upasuaji wa kinamama ulianza mwaka 2015 na kutekelezwa kwa awamu ya kwanza ambapo ujenzi uliishia hatua ya upauaji. Kwa awamu ya pili ujenzi umeendelea mpaka hatua hii ya kukamilika kama inavyoonekana.

Mradi huu wa jengo la upasuaji umegharimu kiasi cha fedha Tshs 117,259,844/=, ambapo Serikali Kuu Tshs 86,184,342/-, Halmashauri Tshs 26,766,285/- na Wananchi Tshs 4,309,217 pamoja na nguvu kazi kwa hatua zote za utekelezaji wa Mradi.

Mradi huu unatarajiwa kuboresha huduma za Afya kwa Wananchi wa Handeni hasa huduma ya upasuaji wa haraka wakati wa kujifungua kwa wateja ambao wangepaswa kusafirishwa hadi Hospitali ya Wilaya, umbali wa Km 57 kutoka hapa.



Mwenge wa Uhuru ukiwa umefika kwenye kituo cha Afya Mkata kwaajili ya kufjungua chumba cha upasuaji kilicholenga kuwasaidia wamama pindi wanapohitaji kujifungua kwa njia ya upasuaji.

Huduma hii itachangia kupunguza vifo vya mama wajawazito/wazazi na watoto wachanga. Aidha wasafiri wanaotumia barabara kuu ya Segera-Chalinze pindi wanapopata ajali za barabarani watanufaika kwa upasuaji mdogo.

Mradi huu utapunguza usumbufu na gharama za kusafirisha wagonjwa wanaohitaji huduma za upasuaji ambazo zinapaswa kupatikana katika ngazi ya Kituo cha Afya kwa mujibu wa miongozo



Baadhi ya Vifaa vilivyopo kwenye jengo la chumba cha upasuaji Kituo cha afya Mkata.



Madaktari na Katibu wa Afya Wilaya mwenye Tshirt nyeupe wakiwa kwenye chumba cha upasuaji kilichokamilika kwa uwepo wa vifaa vyote muhimu kuashiria wapo tayari kuhudumia wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

## Mradi wa tanki la kuhifadhia maji Kata ya Kwamsisi lenye uwezo wa kuhudumia Vijiji vya Kwedikabu na Kwamsisi.

Mradi wa maji kijiji cha Kwedikabu unagharimu kiasi cha Tshs 207,094,411.8/= na unafadhiliwa na Shirika la World Vision kwa kushikiana na Halmashauri ya Wilaya Handeni.

Wananchi wamechangia kupitia nguvukazi ya kuchimba na kufukia mifereji ya urefu wa mita 7,800 ambayo ni sawa na Tshs 13,650,000/=. Baada ya kukamilika mradi huu unategemewa kunufaisha wakazi wapatao 7,059 wa vijiji vya Kwedikabu na Kwamsisi

Mpaka leo tarehe 28/9/2017 hatua ya utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo;-

1. Uchimbaji wa mtaro wa kusambaza maji wenye urefu wa mita 7,800 umefikia asilimia 97%,
2. Ujenzi wa nyumba ya mashine ya kusukumia maji na uzio wake umefikia asilimia 80%,
3. Ujenzi wa mfumo wa umeme wa jua (solar) na kufunga pampu umefikia asilimia 95%
4. Ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji (lita za ujazo 50,000) umefikia asilimia 60%,
5. Ujenzi wa vituo vya kuchotea maji umefikia asilimia 70%




Uwekwaji wa jiwe la msingi kwenye jtanki la kuhifadhia maji unaotarajiwa kunufaisha vijiji vya Kwedikabu na Kwamsisi

## Mradi wa kituo cha Afya kinachojengwa Kata ya Kwamsisi katika kuboresha huduma za afya.

Mradi huu umeanza kutekelezwa mwaka 2017 ambapo mpaka sasa umefikia hatua ya kupandisha kuta. Lengo likiwa ni kuboresha huduma za afya na kusogeza huduma bora za afya karibu na wananchi na kutekeleza Sera ya Afya ya kuwa na kituo cha afya katika kila Kata. Jengo hili likisha kamilika litaweza kutoa huduma za tiba na ushauri kwa wastani wa asilimia 55.

Mradi huu na kwa hatua hii, utakapokamilika utagharimu kiasi cha Tshs 153,000,000/=. Mpaka sasa mradi huu umegharimu kiasi cha Tsh 42,300,000/= Mradi huu unatekelezwa kwa pamoja na Shirika la Word Vision, Halmashauri ya Wilaya ya Handeni na wananchi wa Kata ya Kwamsisi.

Mradi huu unatarajiwa kuboresha huduma za afya kwa wakazi wa Kata ya Kwamsisi inayohudumia vijiji vinne vya Kata ya Kwamsisi ambavyo ni Mkalamo, Pozo, Kwedikabu na Kwamsisi vyenye jumla ya wakazi 12,925.



Jengo la kituo cha afya Kwamsisi kikiwa kimefikiwa na mwenge wa uhuru tayari kwa kuwekewa jiwe la msingi na mkimbiza Mwenge Kitaifa Amour Hamad Amour

## HABARI KATIKA PICHA

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ilitenga Bajeti ya kiasi cha Tshs 96,300,000/ kwa ajili ya kukopesha vikundi vya Wanawake na Vijana lengo likiwa ni kuwawezesha Wananchi Kiuchumi kwa ajili ya kuanzisha miradi midogo midogo ili kuinua kipato cha wanakikundi na jamii kwa ujumla.

Kwa awamu ya kwanza ya mwaka ya 2017/2018 Halmashauri ya Wilaya ya Handeni inatoa mkopo wenye thamani ya Tshs. 13,500,000/= sawa na asilimia 14 ya Bajeti ya mapato ya ndani kwa Vikundi viwili vya Wanawake na Kikundi kimoja cha Vijana. Vikundi hivyo vinajishughulisha na shughuli za ufugaji wa samaki.

Utaratibu uliowekwa ni kwamba, vikundi vilikopeshwa vifaa vya kufugia samaki ambavyo vilikabidhiwa na Mkimbiza mwenge. Baadhi ya vifaa hivyo ni chakula kg 180, vifaranga 3,000 na karatasi maalum kwa ajili ya mabwawa yenye mita za ujazo 70 (m3) katika vikundi . Vikundi vilivyopewa mikopo ni pamoja na:

1) Kikundi cha nguvu kazi vijana chenye wanachama 25 kati ya Wavulana 10 na Wasichana 15,
2) Kikundi cha wanawake Sungura kwanza chenye wanachama 15, na
3) Kikundi cha wanawake cha mafanikio VICOBA chenye wanachama 19.




Mkimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa Ndg.Amour Hamad Amour akizungumza na kikundi cha wananwake.



Mkimbiza Mwenge Kitaifa akipata maelezo ya vifaa vya kufugia samaki kama mkopo kutoka kwa afisa Vijana Mbazi Mfinanga aliyeweka mkono mmoja.



shamra shamra za Ngoma kwenye mapokezi ya Mwenge wa Uhuru kwenye Maabara ya kisayansi Shule ya Sekondari Kwaluguru



Viongozi, wataalamu mbalimbali na Skauti wakiwa tayari kupokea Mwenge na Wakimbiza Mwenge wa uhuru Kitaifa kutoka Handeni Mji.

## HABARI KATIKA PICHA



Halaiki wakishikishwa Mwenge wa Uhuru na Mkimbiza Mwenge Kitaifa na wakimbiza Mwenge wengine kwenye viwanja vya Kwamsisi eneo la Mkesha.



Viongozi na Wataalamu mbalimbali wakiwatayari kusomewa risala ya utii ili shughuli nzima za mkesha ziweze kuanza eneo la viwanja vya Kwamsisi.



Mkimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa Ndg.Amour Hamad Amour akitoa ujumbe wa Mwenge eneo la Mkata.



Mkuu wa Tanga Mh. Martine Shigella Akisoma taarifa ya Mkoa kabla ya kukabidhi Mwenge wa uhuru Pemba Kaskazini.



Kaimu Mkuu wa Wilaya Eng. Gabriel Robert kutoka Lushoto akkikabidhi Mwenge kwa Mkuu wa Wilaya ya Pangani



Wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa wakikabidhiwa rasmi kwa viongozi wa Pemba Kaskazini.